

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE

11

KISWAHILI

Muda: Saa 1:20

MAJIBU

Mwaka: 2024

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **Matano (5)**
2. Jibu maswali **yote**.
3. Andika majibu yote kwenye nafasi zilizoachwa wazi katika kila swali.
4. Andika majibu yote kwa kutumia kalamu ya wino wa **bluu** au **mweusi**

maktaba.tetea.org



SEHEMU A (Alama 10)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Sikiliza kwa makini sentensi zifuatazo kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) **Ngo'mbe wetu ni mkali**

(ii) **Kaka yangu anafua vyuma**

(iii) **Dhahabu nzuri hupatikana Mwadui**

(iv) **Mtoto huyu alifyeka majani**

(v) **Thamanin ya dola imepanda**

SEHEMU B (Alama 10)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

2. Andika neno jipya linaloundwa kwa kudondosha silabi moja katika kila neno ulilopewa.

(i) Mkasi _____

Neno jipya ni **kasi**.

(ii) Wazima _____

Neno jipya ni **wima**.

(iii) Elewa _____

Neno jipya ni **lewa**.

(iv) Mpeni _____

Neno jipya ni **peni**.

(v) Hatibu _____

Neno jipya ni **tabu**.

SEHEMU C (Alama 10)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

3. Andika maana ya nahau katika (i) – (v) kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku na kuliandika katika nafasi iliyoachwa wazi.

Maneno kwenye kisanduku:

tamani kitu, ipo siku utakamatwa, kuishi miaka mingi, ona aibu, mwisho wa safari, fukuzwa kazi, kuiba kitu.

(i) Tia nanga _____

Maana yake ni **mwisho wa safari**.

(ii) Mezea mate _____

Maana yake ni **tamani kitu**.

(iii) Mwaga unga _____

Maana yake ni **ipo siku utakamatwa**.

(iv) Kula chumvi nyingi _____

Maana yake ni **kuishi miaka mingi**.

(v) Ona haya _____

Maana yake ni **ona aibu**.

SEHEMU D (Alama 10)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

4. Kamilisha barua ya kirafiki ifuatayo kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku kisha kuandika katika nafasi zilizoachwa wazi.

Maneno kwenye kisanduku:

Mimi mdogo wako, Madhumuni ya barua, Shule ya Msingi Ushindi, Ni matumaini yangu, Shikamoo.

(i) **Shule ya Msingi Ushindi,**

S. L. P. 773,

Mwanza.

05/05/2024.

Mpendwa Kaka, (ii) **Shikamoo**.

(iii) **Madhumuni ya barua** ni kukujulisha kwamba wote hapo nyumbani hamjambo.

Mimi sijambo na ninaendelea vizuri na masomo.

(iv) **Ni matumaini yangu** kuwa nitakuja kukujulisha kwamba, likizo ya mwezi wa sita nitabaki shuleni ili kujiandaa na Mtihani ya Taifa. Fanya nidemahariri kufaulu vizuri kwa kupata gredi 'A' katika masomo yote.

Ninakutakia kila la kheri katika shughuli zako za kila siku.

(v) **Mimi mdogo wako**,

Akilimali.

SEHEMU E (Alama 10)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

5. Soma kwa makini habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

Kalulu ni kijana anayeishi mtaa wa Kaloleni. Vijana wenzake mtaani walikuwa hawampendi kwa sababu ya tabia zake mbaya za kutowaheshimu wazazi wake, kuvuta bangi na wizi. Tabia mbaya ya Kalulu haikuishia mtaani kwake tu lakini hata shuleni aliendelea na tabia hizo. Walimu wake walijitahidi kumrudi lakini hakutaka kujirekebisha mwishowe alifukuzwa shule.

Siku moja usiku alitoka nyumbani na kwenda kwa rafiki yake aitwaye Mashaka. Yeye pamoja na rafiki yake walikaa kichochozoni wakiwa wanavuta bangi. Polisi walikuwa katika doria walipita katika kichochozoro walichokuwa wamekaa na kuwakamata.

Walipolekwa katika kituo cha polisi na hatimaye mahakamani. Hakimu alitoa hukumu na wote walifungwa katika jela ya watoto kwa miezi sita kwa kosa la kuvuta bangi na uzururaji. Baada ya kumaliza kifungo, Kalulu alibadili tabia na kuwa kijana mtifu sana. Wazazi wake na jamii kwa ujumla walimpenda na kumwamini.

Maswali:

(a) Kalulu ni kijana anayeishi wapi?

Kalulu anaishi **mtaa wa Kaloleni**.

(b) Neno *kumrudi* kama lilivyotumika katika habari uliyosoma lina maana gani?

Neno *kumrudi* lina maana ya **kumsahihisha au kumrekebisha**.

(c) Kwa nini Kalulu na Mashaka walifungwa?

Walifungwa kwa sababu **walivuta bangi na walikuwa wanazurura**.

(d) Taja sababu mbili zilizofanya Kalulu kutopendwa na vijana wenzake.

Sababu ya kwanza ni **kutowaheshimu wazazi wake**.

Sababu ya pili ni **kujihusisha na wizi na kuvuta bangi**.

(e) Habari uliyosoma inatoa funzo gani?

Habari inatufundisha kwamba **tabia mbaya huleta madhara lakini mtu anaweza kubadilika na kuwa mwema**.